



## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MWENENDO WA HALI YA HEWA NCHINI.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inatarajia kutoa mwelekeo wa mvua za msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (Novemba – Aprili), mnamo tarehe 10 Oktoba, 2019. Mvua hizo za msimu ni mahususi kwa maeneo ya mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, kusini mwa mkoa wa Morogoro, Kigoma, Katavi, Tabora, Singida, Dodoma, Lindi na Mtwara.

**HALI YA MVUA:** Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambayo utabiri wake ulitolewa Tarehe 3 Septemba, 2019, mvua za Vuli (OND) 2019 zimeshaanza katika baadhi ya maeneo. Mvua hizo zimeanza mapema katika wiki ya kwanza ya mwezi Oktoba kwa maeneo ya mikoa ya Tanga, Dar es salaam, Pwani pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba. Hali hii inatokana na uwepo wa wimbi anga (Madden – Julian Oscillation (MJO) uliopelekea kuimarika kwa ukanda wa mvua katika kipindi kifupi.

Aidha katika wiki mbili za kwanza za mwezi Oktoba mtawanyiko wa mvua katika maeneo hayo unatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hiyo inatarajiwa kufuatiwa na vipindi vya upungufu wa mvua katika wiki ya tatu ya mwezi Oktoba, 2019.

Kwa upande mwingine, mvua za Vuli katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara zinatarajiwa kuanza katika wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2019 kama ilivyotabiriwa awali. Hata hivyo, maeneo machache ya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha yamepata vipindi vichache vya mvua za nje ya msimu mwanzoni mwa mwezi Oktoba.

**HALI YA JOTO:** Hali ya joto inatarajiwa kuongezeka katika maeneo mengi kadiri msimu wa vuli unavyoendelea.

**USHAURI:** *Wananchi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za utabiri kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na kuzingatia tahadhari zinazotolewa na mirejeo yake na kuzingatia ushauri na miongozo ya wataalam katika sekta husika ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.*

Imetolewa tarehe 04 Oktoba 2019 na:

### Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3

S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)